
# BUNDA Mji

Jan - Machi 2023

Bunda Yetu, Maendeleo Yetu, Tuwajibike | TOLEO NO. 2

# NYATWALI

# KUTWALIWA NA HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI

# YALIYOMO


Nyatwali Kutwaliwa na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti......... UK.1

Baraza Maalumu la kujadli suala la Nyatwali kutwaliwa na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ......UK.4

Mkutano wa kawaida wa baraza la Halmashauri robo ya pili 2022/2023 ........ UK.6

Mafanikio ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan ......Uk.9

Tangazo la viwanja kuuzwa ......UK.14

Matokeo ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 .....UK.15

Ujumbe wa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya mara baada ya kuwasili kituo kipya cha kazi Bunda ...UK.16




# NYATWALI KUTWALIWA NA HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI

Na Liwina Mnamba

MNAMO tarehe 17.11.2022 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kupitia Katibu Tawala wa Wilaya ya Bunda Ndg. Salumu Mtelela alitoa taarifa katika baraza la Halmashauri ya Mji wa Bunda kuhusu mchakato wa kutwaa eneo la Nyatwali kwa manufaa ya Umma na Hifadhi kwamba kupitia Baraza la Mawaziri, Serikali imetoa maamuzi ya Kutwaa  eneo hilo na tayari hatua mbalimbali za kutoa elimu kwa wananchi zimeanza kuandaliwa.

Ghuba ya speke ni eneo la Nywali ambalo limepakana na hifadi ya Taifa ya serengeti pamoja na Ziwa Victoria na mara nyingi kumekua na muingiliano mkubwa wa wanyamapori katika makazi ya watu wa nyatwali.

Mara kadhaa kumekua na matukio ya uharibifu wa mazao utokanao na wanyama pori kama vile tembo, simba, fisi na Mamba kiasi cha kusababisha vifo kwa wakazi wa eneo hilo.

Licha ya wakazi wa eneo hilo kuzoea kuishi na wanyama hao wakali, hawakusita kupiga kelelee kwa Serikali kuona namna ya kudhibiti wanyama hao na kuona namna gani ya kutoa fidia kwa wananchi walioathiriwa na wanyama hao.

Wanyapori wamekua wakilazimika kuingia kwenye makazi ya wananchi kwasababu ya kutafuta chakula pamoja na kufuata maji ziwani.

Baada ya taarifa hiyo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bunda kuhusu maamuzi ya kamati. Hatua za kutoa elimu na kufanya tathimini ya uthamini wa mali za wananchi zilianza katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Baada ya taratibu kukamilika, vikao mbalimbali vya Kutoa elimu vifanyika kwanza kwa viongozi wa Kata ya Nytwali na mitaa yake na kisha kwa wananchi wote Nyatwali.

Timu ya wataalamu wa ardhi na uthamini kutoka Mkoani na Halmashauri ya Mji wa Bunda iliandaa utaratibu mzuri wa kuanza kazi ya uthamini ambapo ailiandaa fomu maalumu ya wananchi waliotayari kuthaminiwa kujaza na kazi ya uthamini kuanza.

Wananchi wengi waliopokea elimu na kuelewa malengo ya Serikali walimiminika kuchukua fomu kujaza na kazi ya uthamini kuanza mara moja. Jambo ambalo wananchi walihakikishiwa ni haki na usawa kwa mali zao wala hakuna atakaeonewa wala kuibiwa.

Zoezi hilo limekua likiendelea na Serikali kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuoan maeneo yenye changamoto kuzitatua. Viongozi wa Serikali za mitaa wamekua msaada mkubwa sana katika kuondoa sintofahamu yoyote ambayo imekua ikijitokeza wakati wa zoezi la uthamini.





Mhe. ANGELINA MABULA
Mwenyekiti wa Kamati

Tarehe 04.01.2023 timu ya Mawaziri nane wa Kisekta iikiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
Mhe. Angelina Mabula ilitua katika ardhi ya Nyatwali kuja kuwaondoa hofu na mashaka iliyokua imetawala kwa wakazi wa nyatwali kuhusu kuhamishwa na stahiki zao.

Jambo la kwanza lililoelezwa na Kamati ya Mawaziri ni kuwafahamisha wananchi kwamba ni kweli Serikali imeamua kutwaa eneo hilo kwa manufaa makubwa ya Taifa na Usalama wa Wananchi dhidi ya wanyama wakali wa porini.

Pili, Kamati iliwaondoa hofu wananchi juu ya stahiki zao na mahali watakapokwenda mara baada ya kuhamishwa. Walisema Serikali imejipanga kuhakikisha huduma zote za msingi zinakuwepo kama zilizvyokuwepo mahali hapo walipokua wanaishi.

Aidha, Kamati iliongeza kuwa huduma za Afya, Elimu, Ufugaji, Kilimo na Umwagiliaji pamoja na huduma ya maji vitapewa kipaumbele katika makazi mapya watakapohamia wananchi hao bila kuathiii huduma za kiuchumi.

Mhe. Mabula aliongeza kusema kuwa Serikali haitawabeba na kuwapeleka sehemu fulani na badala yake baada ya uthamini na malipo kufanyika Serikali itawaelekeza maeneo ambayo ambayo yametengwa ambayo mwananchi atachangua ni wapi ahamie, yaweza kuwa ndani ya Mkoa wa Mara au nje ya mkoa.

Kamati pia iliweka sawa kuhusu maneno potofu yanayosambaa kwamba kuna Mwekezaji anayekuja kuchukua eneo hilo kuwa taarifa hizo si za kweli na zipuuzwe hakuna Mwekezaji yeyote atakayepewa eneo hilo.

Mwisho, Kamati imewataka wanachi wa Nyatwali kuwa watulivu wakati Serikali ikiendelea na zoezi la uthamini na kwamba kila mwananchi atalipwa kulingana na sheria, taratibu na kanuni za nchi bila kumuonea mtu yeyote. Gharama za uthamini wa vitu tayari wananchi walishaelezwa na zimebadikwa katika mbao za matangazo.

# PICHA MBALIMBALI ZA MKUTANO WA KAMATI YA MAWAZIRI NANE WA KISEKTA KUHUSU SUALA LA NYATWALI KUTWALIWA



Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee
Mkuu wa Mkoa wa Mara



Mhe. Joshua Nassari
Mkuu wa Wilaya ya Bunda (Wakati huo)



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya ya Bunda Pamoja na Wataalamu kutoka Mkoani na Wilayani wakifatilia Kikao cha ndani cha Kamati ya Mawaziri nane wa Kisekta





WANANCHI WA KATA YA NYATWALI
WAKIFATILIA MKUTANO

# BARAZA MAALUMU LA KUJADILI SUALA LA NYATWALI KUTWALIWA NA HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI



Na Liwina Mnamba
Tarehe 22.02.2023

Kupitia Baraza Maalumu la Halmashauri ya Mji wa Bunda la Kupata taarifa ya mchakato wa kutwaa eneo la Nyatwali na Serikali kwa manufaa ya Umma, Mhe. Dkt. Vicent Anney Mkuu wa Wilaya ya Bunda ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia huu mchakato wa kutwaa hilo eneo amewatoa hofu wakazi wa Nyatwali juu ya stahiki zao katika zoezi linaloendelea la uthamini wa mali zao na kwamba kila mmoja atapata stahiki zake bila kuonewa.

Mheshimiwa Anney amesema Serikali haitamuonea mwananchi yeyote na haina lengo la kumsumbua mwananchi na ndio maana kupitia maamuzi ya Baraza la Mawaziri ya kutwaa eneo hilo la Nyatwali, Serikali iimetafuta fedha kwaajili ya kuwafidia wananchi ili waweze kujimudu huko watakakokwenda.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ametoa ufafanuzi kuhusu malalamiko ya fedha za fidia kuwa ndogo, barabara inayokatisha eneo hilo, mustakabali wa eneo la Mjapani na eneo la malisho pamoja na maeneo ya wazi ya kuwa mambo yote hayo yamechukuliwa na kamati yake kwaajili ya majadiliano kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wanaohusika na jambo hilo.

Manthalani, Mheshimiwa Anney amewataka Viongozi kudumisha, amani, umoja na utulivu wakati suala hili likiwa linafanyiwa kazi na mchakato wa uthamini ukiwa



Mhe. Dkt Vicent Naano Anney
Mkuu wa Wilaya ya Bunda

unaendelea na amesisitiza kwamba asitokee mtu yeyote wa kuhamasisha au kuchochea vurugu. Ameeleza kuwa, ni vema wananchi na viongozi wadai haki kwa kufuata sheria na kujenga hoja.

Awali, Waheshimiwa Madiwani walihoji mambo mbalimbali kutaka kujua jinsi mchakato huu unavyoenda, stahiki za watu wa Nyatwali kwa kuzingatia uhalisia wa hali ya maisha na kwa kuangalia ubinadamu, haki katika uthamini wa mali zao na utaratibu utakaotumika katika maeneo ya wazi na malisho.

Naye Mwenyekiti wa Halmasahuri ya Mji wa Bunda Mhe. Michael Kweka aliwahakikishia Waheshimiwa Madiwani kuwa wako pamoja katika suala hilo hadi zoezi litakapokamilika na kuhakikisha Wananyatwali wanapata haki yao na kuwapokea katika maeneo watakayohamia.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda Ngd. Emmanuel Mkongo alitoa shukrani kwa Wataalamu kwa ufafanuzi mzuri uliozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika suala hilo na kuondoa sintofahamu kwa wajumbe wa Baraza.



Mhe. Michael Kweka
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bunda



Ngd. Emmanuel Mkongo
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda



Baadhi ya Waheshimiwa Madiwani wakifatilia Majadiliano ya Mkutano wa Baraza

# MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA HALMSHAHAURI YA MJI WA BUNDA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI ROBO YA PILI 2022/2023

**Na Liwina Mnamba**
**02.03.2023**

Mkutano wa kawaida wa Baraza la Halmashuri ya Mji wa Bunda limekaa kuleleza shughuli za utekelezaji robo ya Pili 2022/2023 ambapo Kamati nne za Halmashauri ziliwasilisha zinazoangazia Divisheni zilizopo chini yao.

Kamati hizo ni Kamatai ya Fedha na Utawala, Kamati ya Mipango Miji, Kamati ya Elimu, Afya na Uchumi pamoja na Kamati ya UKIMWI. Baada ya Taarifa hizo kuwasilishwa wajumbe walizipokea na kupata wasaa wa kujadili kwa kina taarifa pale ilipobidi.

Kupitia Baraza hilo, Wajumbe walipata nafasi ya kujadili suala la mlima Kaswaka ambapo wajumbe walikubalina kwamba suala hilo Wataalamu walifanyie kazi haraka na kuwasilisha mapendekezo katika vikao vya kisheria kwaajili ya kutolewa maamuzi.

Aidha wajumbe walitaka kufahamishwa juu ya mradi wa kulima barabara unaofanywa na walengwa kwamba ni mpango wa Halmashuri au Kitaifa ambapo majibu yalitolewa kwamba mpango huo ni wa kitaifa ulioletwa na TASAF ikiwa na lengo la kuwakumbusha walengwa kwamba wanatakiwa kujishughulisha na kazi mbalimbali zinazoweza kuwaingizia kipato na si kukaa tu kusubiri fedha za kunusuru kaya masikini.



Hata hivyo, wajumbe wameshauri elimu kuendelea kutolewa kwa walengwa ili kuondoa mitazamo hai iliyojengeka vichwani mwa wengi. Aidha, uongozi umekiri kuchelewa kwa vifaa vya mradi huo kutokana nasababu mbalimbali zisizoweza kuzuilika jambo lililopolekea walengwa wengi kutumia vifaa vyao.

Baraza hili lilieleza pia kuhusu kuchelewa kwa fidia za wananchi walioharibiwa mazao yao na tembo kwamba suala hilo lilishafikishwa katika Wizara husika na sasa kinachoendelea ni kuandika barua za kukumbusha na pindi yatakapokuwa tayari basi wananchi hao watalipwa fidia zao.

Kupitia Baraza hili, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda ndg. Emmanuel Mkongo alitoa taarifa kwa ufupi kuhusu bakaa iliyopatikana katika ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza kutokana na manunuzi ya jumla (Bulk procurement) ya mbao na bati.

Mkurugenzi alieleza kuwa Halmashauri imefanikiwa kuokoa kiasi cha fedha ambacho kitawasilishwa katika Kamati ya fedha na Utawala kwaajili ya kupangiwa matumizi na kuelekezwa kwenye shule za sekondari zenye changamoto.

Mbali na Taarifa ya utekeleza ya Halmashauri, Taasisi tatu zinazofanya kazi moja kwa moja na wananchi wa Bunda zilipata nafasi ya kuwasilisha taarifa yao ya utekelezaji kama ifuatavyo:

TARURA



Mamlaka ya Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) kupitia kwa Mhandisi Michael alisema kuwa Bajeti iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni Bilioni 2.09. bajeti hii inaendelea kutekelezwa hadi sasa kwa kukarabati na kutengeneza barabara zote zilizowekwa kwenye bajeti.

Aidha Mhandisi Michael amewatoa hofu na mashaka Waheshimiwa Madiwani kwamba barabara zote zitafanyiwa kazi na kwa zile ambazo hazimo kwenye bajeti hii zimezingatiwa katika bajeti ijayo ya mwaka 2023/2024.

BUWSSA



**BI. ESTHER GILYOMA**
**KAIMU MKURUGENZI BUWSSA**

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Bunda Bi. Esther Gilyoma alipata nafasi ya kuelezea hatua ya utekelezaji iliyofikiwa na Taasisi yake robo ya pili 2022/2023/

Bi. Esther Gilyoma amesema kwa mwaka wa fedha huu walikua na miradi kadhaa ya ambayo wanaitekeleza na kuimalizia. Miradi hiyo ni Chujio la maji Nyabehu ambapo mradi umefikia asilimia 99.

Mradi mwingine ni mradi wa Tenki la maji Misisi Zanzibar ambao tayari wananchi wameshaanza kutumia maji. Miradi mingine ambayo wanatarajia kumalizia mwaka huu wa fedha ni mradi wa Manyamanya Mgaja na Balili Kunzugu.

Aidha Kaimu Mkurugenzi ameongeza kusema kuwa wanatarajia kutekeleza miradi mikubwa ambayo ni Mradi wa kuhifadhi maji taka eneo la Butakale na Mradi wa Tenki la maji la cubic meter 400 katika eneo la mlima Kilimahewa.

TANESCO

Katika wasilisho la shirika la umeme Tanzania (TANESCO) limesema miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa mwaka 2022/2023 ni mradi wa Kilimahewa Mara lint ambapo tayari umeme unawaka, mradi wa Manyamanyama Mbugani, Mradi wa Rwabu na mradi wa Kilimahewa juu. Katika miradi hiyo kitu kilichobaki ni waya ili kuunganisha umeme.

Aidha kuhusu mradi wa REA, Mhandisi amesema tayari mitaa yote isiyo na umeme taarifa zao zimewasilishwa kwaajili ya kuwekwa kwenye bajeti.



# MIAKA 2 YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MADARAKANI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

## SEKTA YA AFYA

## 2023


Hospitali mpya ya Halmashauri ya Mji


Kituo cha Afya Wariku


MIAKA 2 YA MAMA


Jumla ya Zahanati 6 zimekamilishwa


X-RAY


DKT. VICENT NAANO
DC BUNDA


Nyumba ya Watumishi 3 in 1


EMMANUEL MKONGO
MKURUGENZI

# HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA TUNASEMA ASANTE MAMA

OFISI YA MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

## MIAKA 2 YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MADARAKANI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

### SEKTA YA MIUNDOMBINU YA BARABARA

# 2023



DKT. VICENT NAANO
DC BUNDA





MIAKA 2 YA MAMA



Sehemu ya barabara ya Kisorya - Mugumu katika Halmashauri ya Mji wa Bunda





EMMANUEL MKONGO
MKURUGENZI

## HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA TUNASEMA ASANTE MAMA

OFISI YA MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

# MIAKA 2 YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MADARAKANI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

## SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

## 2023

| SHULE | DRS | TSH. (000,000/-) |
|---|---|---|
| 1. Bunda sek | 2 | 40 |
| 2. Migungani sek | 8 | 160 |
| 3. Sizaki sek | 3 | 60 |
| 4. Bunda stoo | 10 | 200 |
| 5. Manyamanyama | 5 | 100 |
| 6. Sazira sek | 8 | 160 |
| 7. Kabasa sek | 1 | 20 |
| 8. Rubana sek | 10 | 200 |
| 9. Nyiendo sek | 4 | 80 |
| 10. Dr. Nchimbi | 10 | 200 |
| 11. Guta sek | 13 | 260 |
| 12. Wariku sek | 1 | 20 |
| 13. Paul Jones | 2 | 40 |

JUMLA YA MADARASA 77

JUMLA YA FEDHA - BILION 1.54



MIAKA 2 YA MAMA



SAZIRA SEK



BUNDA STOO SEK



DKT. VICENT NAANO
DC BUNDA



DR. NCHIMBI SEK



EMMANUEL MKONGO
MKURUGENZI

# HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA TUNASEMA ASANTE MAMA

OFISI YA MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

# MIAKA 2 YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MADARAKANI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

## SEKTA YA ELIMU - VYOO MAPATO YA NDANI

## 2023



S/M MAKALEKALE
MATUNDU SITA - Mil 7.5



S/S SAZIRA
MATUNDU 9 - Mil 10.58



MIAKA 2 YA MAMA



S/S BUNDA
MATUNDU 12 - Mil 12.17



S/M LIGAMBA
MATUNDU 6 - Mil 7.54



DKT. VICENT NAANO
DC BUNDA



S/S DR. NCHIMBI
MATUNDU 6 - Mil 6.47



EMMANUEL MKONGO
MKURUGENZI

**HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA
TUNASEMA ASANTE MAMA**

OFISI YA MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA



**MHE.DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

*Miaka 2 ya Mama*

Uongozi, Watumishi na Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda tunakupongeza kwa Uongozi Imara, Hodari na Thabiti katika kuleta Maendeleo nchini.

*Kazi iendeleee...*

# VIWANJA VINAUZWA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anapenda kuwatangazia wananchi wote kwamba Viwanja vya Makazi, Makazi na biashara na vya Biashara vilivyopimwa vinauzwa.

## ENEO

Bunda stoo Mtaa wa Idara ya Maji karibu na Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Shule ya wasichana ACT Bunda, Zahanati ya Dimmese sisters na Viwanda vya Villian.

## GHARAMA

(Square mita)

1. Makazi - Tsh. 2,200/-
2. Makazi na Biashara - Tsh. 2,300/-
3. Biashara - Tsh. 2,500/-

**Huduma zote muhimu zinapatikana, Umeme, Maji na Barabara**

**Kwa Maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia simu namba:**

| AFISA ARDHI | AFISA MAPATO | AFISA HABARI |
|---|---|---|
| 0757958004 | 0688913313 | 0765889459 |

*Tembelea pia www.bundatc.go.tz*

# Hongera Bunda Mji

## MATOKEO YA MWENGE WA UHURU 2022

Halmashauri ya Mji wa Bunda imefanikiwa kuwa ya:

**1** Kimkoa kati ya Halmasauri 9

**2** Kikanda kati ya Halmashauri 43

**17** Kitaifa kati ya Halmashauri 188

Menejimenti inapenda kutoa pongezi na shukrani kwa Viongozi wa Wilaya, Wafanyakazi, Wadau na Wananchi wote kwa ushirikiano katika kufanikisha jambo hili.



Hongera wanabunda kwa ushindi huu mnono mlioupata

Umoja, Mshikamano na ushirikiano ndio nguzo ya ushindi.

Pamoja tunaweza

# UJUMBE WA MKUU WA WILAYA DKT. VICENT ANNEY MARA BAADA YA KUWASILI KITUO KIPYA CHA KAZI WILAYANI BUNDA












HALIUZWI


**NDG. EMMANUEL J. MKONGO**
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA
td@bundatc.go.tz

**LIWINA J. MNAMBA**
KAIMU MKUU WA KITENGO
MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA
0756889459